

Hatua za kiusalama zinazozingatiwa katika matumizi ya vifaa vya kidijitali

- a) Kuomba idhini kwa mwalimu, mzazi au mlezi kabla ya kutumia vifaa vya kidijitali.
- b) Kutazama filamu na kusoma matini kwenye mtandao usio salama.
- c) Kutambua mtandao salama wenye matini unayohitaji.
- d) Kutambua jina la faili unayohitaji yenye mada lengwa.
- e) Kutumia vifaa vya kidijitali bila idhini hadi usiku wa manane.
- f) Kutambua jinsi ya kufungua na kuifunga faili.
- g) Kutowasiliana na watu msiowajua mtandaoni.
- h) Kutomwambia mwalimu, mzazi au mlezi wako unapopata ujumbe kutoka kwa mtu usiyemjua mtandaoni.
- i) Kuwajibika mtandaoni kama vile kutosakura mitandao usioijua na kutotoa habari za kibinafsi kwa watu mitandaoni.
- j) Kutoa habari kwa mwalimu, mzazi au mlezi unapopata ujumbe kutoka kwa mtu au watu msiowajua mtandaoni.

**Kuandika: aina za insha: barua rasmi**

**Kutambua barua rasmi**

**Kusoma barua rasmi ili kutambua vipengele vyake**

MARIA JUHUDI (GREDI YA SITA),  
S. L. P. 548,

MUSANDA.

17 - 11 - 2020

MWALIMU MSIMAMIZI,  
KLABU YA UIGIZAJI,  
S. L. P. 548,  
MUSANDA.

Kwa Bwana / Bibi,

KUH: KUOMBA RUHUSA YA KUJIUNGA NA KLABU YA UIGIZAJI  
SHULENI

Jina langu ni Maria Juhudi, mwanafunzi wa gredi ya sita katika shule hii. Tangu nilipojiunga na shule hii mwaka uliopita, nimevutiwa sana na shughuli za Klabu ya Ugizaji unayoiongoza. Ninachukua fursa hii kuomba nafasi ya kujiunga na klabu hiyo. Nina talanta ya uigizaji inayohitaji kukuzwa. Bila shaka, shughuli za klabu hii na ushauri wako utanifaa sana.

Nina matarajio makubwa kuwa utalikubali ombi langu. Pokea shukrani za dhati kutoka kwangu kwa kuutenga muda wako ili kuusoma waraka huu. Kwaheri.

Wako mtiifu,  
**juhudimaria**

MARIA JUHUDI

SURA YA 5: MSHIKAMANO WA KITAIFA: kutambua insha za maelezo

#### UMUHIMU WA UMOJA WA KITAIFA

Umoja ni hali ya kufanya mambo kwa ushirikiano bila kujitenga. Mambo mengi mno huweza kufanyika vizuri iwapo kuna ushirikiano baina ya wahusika. Kujaribu kujifanyia mambo bila kusaidiana na wengine si jambo zuri. Je, umoja wa kitaifa una umuhimu gani? Jambo la kwanza, umoja wa kitaifa huleta ushirikiano baina ya wananchi. Ushirikiano huu huwa katika nyanja mbalimbali kama vile kazini, katika biashara na michezoni. Watu wanaposhirikiana katika shughuli zao, bila shaka wao hufaulu.

Aidha, umoja huimarisha amani katika nchi yetu. Amani ni muhimu sana katika nchi. Vita na chuki ni adui mkubwa sana kwa taifa hili. Nchi yenye amani hupiga hatua katika kila sehemu. Vita huharibu mali pamoja na watu kupoteza maisha. Kwa hivyo, ni vyema kuhakikisha kuwa tunaishi kwa amani na umoja. Pakitokea kosa lolote kati yetu, ni vizuri kuzungumza na kuelewana. Kusameheana ni jambo muhimu sana. Unapokosewa na mtu yeyote, kumbuka kuwa wewe pia hukosea. Wakenya tupendane na kuishi kwa amani.

Kadhhalika, umoja huiwezesha serikali kushughulikia mambo muhimu ya taifa. Badala ya kutumia rasilmali za nchi katika kukabiliana na uhalifu, serikali hutumia muda wake kulijenga taifa. Katika nchi ambayo haina umoja, serikali hutumia wakati mwingi kuwatuliza wananchi na kuwaeleza kuhusu umuhimu wa kuwa na ushirikiano. Katika hali hiyo, maendeleo hurudi chini. Tunapoishi kwa amani, serikali yetu hutumia pesa na wakati wake kushughulikia mambo mengine.

Umoja wa kitaifa huchangia mno katika maendeleo ya kitaifa. Katika nchi yenye umoja, wananchi hushirikiana katika shughuli zao. Kwa hivyo, ni rahisi sana kufaulu katika kila walifanyalo. Kufaulu katika kazi na biashara huwapa wananchi pesa. Pesa hizo hutumika kuanzishia miradi mingine ya maendeleo. Vilevile, ushuru ambao hulipwa na wafanyakazi na wafanyabiashara hutumiwa na serikali katika ujenzi wa barabara, hospitali na kadhhalika.

1. Insha mliyoisoma mtandaoni ni ya aina gani?
2. Umoja wakitaifa una umuhimu gani kulingana na insha hiyo?
3. Jadilini faida zingine za umoja wa kitaifa ambazo hazijajadiliwa katika insha hiyo.

### **SURA YA 11: Ushuru: kutambua maudhui katika barua rasmi**

BIDII BAKARI,  
SHULE YA BUSARA,  
S. L. P. 802,  
MUMIAS.

16 - 10 - 2021

MWENYEKITI,  
Klabu ya MJADALA,  
SHULE YA ELIMU BORA,  
S. L. P. 48,  
KILIMANI.

Kwa Bwana / Bibi,

**KUH: KUWAALIKA KATIKA MJADALA**

Jina langu ni Bidii Baraka, katibu wa chama cha mjadala katika shule ya Busara. Ninachukua fursa hii kwa niaba ya chama kualika chama chenu katika mjadala kwenye shule yetu. Mjadala huo utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 30-10-2021, kuanzia saa nne asubuhi. Tumetenga saa na siku hii ili kuwapa wanafunzi nafasi nzuri ya kusafiri na kushiriki. Mada ya mjadala itakuwa **TEKNOLOJIA IMELETA MANUFAA MENGI KULIKO HASARA.**

Ni matarajio yetu kuwa mtalikubali ombi letu. Iwapo ombi letu litakubalika, tunaomba mtupe maoni kuhusu iwapo mngenda kuunga mkono au kuupinga mjadala huo. Vilevile, mna uhuru wa kupendekeza mada nyingine tofauti tutakayojadili katika mjadala wa wakati ujao. Tunawatakia kila la heri katika shughuli zenu za masomo.

Wenu mwaminifu,

**Bbaraka**  
BIDII BARAKA (Katibu)